

ASb
approved



Kiswahili

Anansi, Kunguru Na Mamba

Mutugi Kamundi
Wiehan de Jager



Wakati mmoja kulikuwa na kiangazi na njaa kubwa. Hakuna aliyekuwa na chakula isipokuwa kunguru. Kila asubuhi walikwenda mbali kwenye mti uliokuwa na matunda matamu ya mkuyu uliokuwa katikati ya mto. Kisha walirudi huku wamebeba matunda ya mkuyu kuwaletea ndugu zao. Alipoyaona matunda hayo, Buibui Anansi alidondokwa na mate. Je, angwezaje kuyapata matunda hayo?



Alifikiri, akafikiri, na akapata wazo zuri. Alijipaka nta inayonata kwenye sehemu yake ya nyuma. Kisha akachukua kigae cha nyungu akaenda kwa kina kunguru. "Tafadhalii naomba usadizi!" alisema. "Naomba kaa la moto. Jiko langu limezimika." Walipokuwa wakimchukulia kaa la moto kutoka kwenye jiko, Anansi alikalia tunda moja kubwa la mkuyu. Tunda hilo lilijinata kwenye makalio. Aliwashukuru kunguru na kuharakisha kwenda nyumbani kufurahia kuyu hilo.



Lakini tunda moja halikutosha. Alirudi kwa mara ya pili akafanya vile aliquwa amefanya tena. Aliporudi mara ya tatu kunguru walianza kumshuku. "Kwa nini unarudi hapa mara kwa mara kuomba kaa la moto?" waliuliza. Anansi akajibu, "kila wakati nikifika nyumbani kaa huwa limezimika." "Unatudanganya!" Kunguru walimwambia. "Una tamaa ya chakula chetu." "Si kweli", Anansi akasema. Halafu akaanza kulia. Kunguru wakamwonea huruma sana. "Sawasawa," Kunguru wakasema. "Beba kaa jingine la moto, na kesho mapema asubuhi tutaenda nawe kwenye mkuyu wenye matunda."



Asubuhi iliyofuata kila kunguru alimchangia Anansi manyoya akapata mbawa. Basi akaruka hadi kwenye mkuyu uliokuwa katikati ya mto. Alipoona matunda yale matamu aliyataka yote peke yake. Kila wakati kunguru alipojaribu kuchuma tunda, kunguru alisema, "Wacha, hilo ni langu! Mimi nililiona kwanza!" Halafu alichukuwa kila tunda na kuliweka ndani ya mfuko wake. Hatimaye, alichukuwa matunda yote na kunguru hawakupata chochote.



Aliachwa peke yake, giza likaanza kutanda. "Siwezi kuishi kwenye huu mti maisha yangu yote," alijambia, "ni lazima niruke hewani kama kunguru. Basi akashusha pumzi, kisha akaruka, na mara CHUBWI! Akaanguka ndani ya mto baina ya mamba hatari."



"Hapa tuna nyama tamu na nyororo." Mamba mmoja alisema. "Tuanze mlo mm. Nyum." "Tafadhali, msiniue," Anansi akasema. Kisha akaanza kulia. "Kwani hamjui mimi ni mmoja wenu? Nilipotea wakati wa mababu zenu na hakuna aliyeweza kunipata. Sasa nyinyi ni ndugu zangu!" Alilia machozi hadi mamba wakamwonea huruma.




Lakini mamba mzee hakuamini, "Tutajua kwamba wewe ni mmoja wetu ukiweza kunywa supu ya matope kama sisi." Walimpatia kibuyu cha maji machafu. "Nyanyangu alikuwa akitengeza supu kama hii," Anansi alisema. Lakini alichimba shimo kwenye ardhi akitumia mguu wake wa nyuma, kisha akatoboa shimo kwenye kibuyu kwa mguu wake wa mbele. Alijifanya kwamba alikuwa akinywa yale maji na kumbe yalikuwa yakimwagika kupitia katikati ya miguu yake. "Tamu sana!" alisema huku akirudisha kibuyu.



"Sasa tumejua wewe bila shaka ni mmoja wetu," mamba wakamwambia. Kwa hivyo walimruhusu Anansi kulala pamoja nao usiku huo. "Kesho asubuhi nitawaambia hadithi kuhusu maisha yangu," Anansi aliwaambia walipokuwa wakianza kulala.



Siku iliyofuata, Anansi alimaka asubuhi na mapema akamwamsha mamba mmoja. "Ningependa kwenda nimlete mke na watoto wangu ili wanisaidie kuhadithia. Je, utanisaidia niende kuwaleta kabla ya wengine kuamka?"



Mamba huyo hakufurahi kwa kuamshwa mapema sana. "Tafadhali nisaidie! Wewe unajua kuogelea haraka kuliko mimi," Anansi akamwambia. Mamba akakubali kumbeba Anansi kwenye pua lake hadi ukingoni mwa mto. Anansi alishuka kutoka kwa pua la mamba akasema, "Nitarudi hivi punde. Tafadhali ningojepapo hapo!" Kisha akatorokea kwenye nyasi haraka haraka.



Tangu siku hiyo, mamba angali
anamngoja Anansi kwenye ukingo wa
mto, pua na macho yake makubwa
yakijitokeza juu ya maji.

You are free to download, copy, translate or adapt this story and use the illustrations as long as you attribute in the following way:

Anansi, Kunguru Na Mamba

Author - Ghanaian folktale

Translation - Mutugi Kamundi

Illustration - Wiehan de Jager

Language - Kiswahili

Level - Longer paragraphs

© African Storybook Initiative 2014

Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org